KENYA SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT.

GREDI YA SABA

MUHULA WA TATU.

KISWAHILI.

Jina:_____

Gredi:_____ Tarehe:_____

Maswali	**Alama**	**Alama ya mwanafunzi**

Maagizo.

a) Andika jina shule nambari ya usajili kwa nafasi uliopewa.

b) Andika tarehe kwenywe nafasi iliyoachwa.

c) Jibu maswali yote kwenyw nafasi uliyopewa.\maswali yote yajibiwe kwa kiswahili.

SEHEMU A: UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kisha uandike ufupisho wake.

Maji ni muhimu katika Maisha ya binadamu, Wanyama, ndege, Samaki, wadudu n ahata mimea. Ni kweli kuwa maji ni uhai. Maji hupatikana baharini, maziwani, mitoni n ahata visiwani. Matumizi yam aji ni kama vile: kupikia, kuoshea, kunyunyizia mime ana kuwapa mifugo kunywa. Maeneo ya nchi ambayo hayana mito au mvua hayavutii watu wengi kuishi huko. Wenyeji wa sehemu hizo hukabiliwa na ukame.

Milima, misitu na maziwa huwa na vianzo vya mito. Mlima Kenya huwa na chanzo cha mto Tana nayo milima ya Cherangani na milima Elgon ni vyanzo vya mto nzoia. Mito hii ni miongoni mwa mito muhimu katika nchi ya Kenya. Faida ya mito hii ni chungu nzima. Hutupatia maji ya matumizi nyumbani na viwandani, mito mingine hutumika kuzalisha nguvu za umeme na usafiri pia. Maji haya ya mito pia hunywewa na Wanyama na vilevile huvutia watalii. Hivyo basi tunastahili kuyatunza maeneo mbalimbali ya maji.

Tusiharibu misitu kwa kukata miti kiholela. Ikiwa tunakata mti mmoja, tupande miwili au Zaidi. Ni jukumu la kila mmoja kuyalinda mazingira yetu. Tusitupe takataka ovyo ovyo. Mvua inaponyesha huyabeba takataka zilizo tapakaa hadi katika mito. Wajenzi waviwanda wanatahadharishwa dhidi ya kuelekeza majiaka katika mito na maziwa.

Andika ufupisho wa kifungu hiki kuhusu umuhimu wa maji. Zingatia yafuatayo; Maneno yasizidi 60 na iwe katika mpangilio wa kuendelea. Ikiwa aya moja tu.

1. Tumia maneno yako mwenyewe bila kughairi maana ya kifungu chenyewe. (Al.10)